

Maswali

1. Mbona wanafunzi walikuwa na furaha?
2. Yesu aliwaambia wanafunzi wafanye nini?
3. Yesu aliwapeleka wanafunzi wapi?
4. Nini ilifanyika kwa Yesu kule?
5. Nani aliwakujia wanafunzi?
6. Malaika waliwambia wanafunzi nini?
7. Wanafunzi walifanya nini?
8. Yesu atafanya nini atakaporudi hapa duniani?
9. Ufalme wa Mungu utakuwaje?
10. Yesu anataka tufanye nini?

Majibu

1. Walifurahi kwa sababu Yesu alikuwa hai tena.
2. Yesu aliwaambia waambie wengine kwamba yu hai tena.
3. Yesu aliwapeleka wanafunzi kwa Mlima wa Mzeituni.
4. Yesu alienda juu angani kuishi na Mungu.
5. Malaika wawili waliwakujia wanafunzi.
6. Waliwaambia kwamba Yesu atakuja tu vile ameenda.
7. Wanafunzi walijitahidi kuambia kila mtu kuhusu Ufalme wa ajabu wa Mungu utakaokuwa Duniani
8. Yesu atakuwa Mfalme wa ulimwengu wote na atatawalia Yerusalemu
9. Utakuwa wa ajabu, kila mtu atakaa vema na furaha, chakula kingi na sheria za Mungu.
10. Yesu anataka tuwe tayari na tumtii

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

46 Yesu atarudi tena

Marejeo

Matendo ya Mitume 1: 1—11

Kiini cha somo

Yesu amepaa Mbinguni atakuwa huko mpaka wakati utimie wa kurudi duniani


Maneno maalum

1. Wanafunzi + sema habari njema + Yesu yu hai + Yesu atasaidia.
2. Yesu + wanafunzi + mlima wa Mzeituni.
3. Yesu + anga + mawingu + Malaika wawili + Yesu atarudi.
4. Wanafunzi + furaha + ahadi za Mungu + jitahidi.
5. Yesu + karibu atakuja + ufalme wa ajabu.
6. Kuwa tayari + hitajika huko.

46.1 Mitume na marafiki wa Yesu walikuwa na furaha kubwa sana kwa sababu ya Mungu kumfufua Yesu. Yesu sasa alikuwa anakwenda kuishi mbinguni akiwa pamoja na Baba yake, Mungu. Lakini kwanza Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwenda kuwaambia wengine habari njema za mwujiza mkubwa ambao Mungu aliufanya kwa Yesu kuwa hai tena milele na milele, na kuwa siku moja atauweka ufalme wa Mungu hapa duniani. Yesu aliwaahidi wanafunzi wake atawasaidia kufanya mapenzi yake ingawaje yeye kwa muda huo hatakuwepo pamoja nao hapa duniani.

46.2 Siku moja, ambao ulikuwa ni muda wa Yesu kwenda kuishi pamoja na Mungu mbinguni. Ndipo Yesu akaenda pamoja na wanafunzi wake hadi kwenye mlima wa mzeituni, karibu na Yerusalemu. Akiwa pale mlimani aliwaambia kazi ambayo itawabidi waifanye kwa ajili yake.

46.3 Na kasha, ghafula, Yesu akanyanyuliwa kutoka pale mlimani. Akaenda juu mawinguni na kwa ajili ya mawingu Yesu hakuweza kuonekana. Wanafunzi wake wakaendelea kutazama juu mbinguni. Ndipo waliposikia mmoja akizungumza nao, wakageuka wakawaona malaika wawili wakiwa wamevaa mavazi meupe nao waliwaambia kuhusu ahadi za Mungu. Mungu aliahidi kuwa siku moja Yesu atarudi tena duniani na akiwa kama vile walivyomwona alipokuwa akienda zake mbinguni.



46.4 Wanafunzi waliposikia ahadi ya Mungu walifurahi sana. Wote walifanya kazi kwa bidii wakiifanya kazi ambayo Yesu aliwaagiza waifanye. Walimwambia kila mtu kuhusu habari za Yesu na kuhusu ufalme mzuri wa ajabu ambao atauweka hapa duniani.

46.5 Tunautazamia muda ambapo Yesu atarudi tena hapa duniani kuwa Mfalme. Yesu atarudi hivi karibuni, wakati Yesu atakaporudi ataketi katika kiti cha enzi katika Yerusalemu na atakuwa Mfalme wa dunia yote. Yesu ataifanya dunia hii kuwa mahali pazuri sana pa kuishi. Atawaponya watu wote wagonjwa na kila mmoja atakuwa ni mwenye furaha. Ataleta wingi wa chakula kuweza kustawi ili kila mmoja awe na chakula kingi.

Yesu atawafundisha watu kuishi kwa kufuata sheria za Mungu, na kwa hiyo hakutakuwepo vita tena kama ilivyo leo. Hata wanyama wa (mwitu) porini watakuwa ni marafiki wa binadamu. Hakuna hata mmoja ambaye ataishi kuwa na hofu katika Ufalme wa Mungu.

46.6 Bwana Yesu, atarudi upesi sana, na anataka sisi tuwe tayari kwa ajili yake. Kama tukimtii ndipo tutakapokuwa rafiki zake na tutaweza kuingia katika Ufalme wake. Ninataka kuwa rafiki wa Yesu na niweze kuishi katika Ufalme mzuri sana wa Mungu, na wewe je! Unataka?

